

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

(Barua Zote Ziandikwe Kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA RUKWA

TEL:025-2802429

FAX:025-2802796

Email:ded@kalambodc.go.tz

Kumb.Na.KDC/L.40/14/86



S. L. P. 3
MATAI
KALAMBO
TANZANIA

21/03/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **38** za Watendaji wa Vijiji daraja la III

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne(IV) au sita (VI).
- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala,Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa Fedha,Maendeleo ya Jamiii na Sanaa kutoka Chuo Cha Serikali za Mitaa **Hombolo** au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

2. MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali, yaani **TGS 'B'**

3. MAJUKUMU YA KAZI

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji

- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- III. Kuratibu na Kusimamia Upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- IV. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu mbalimbali za Serikali
- V. Kukusanya, kusimamia na Kutunza Nyaraka na Kumbukumbu zote za Kijiji
- VI. Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa Umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- VII. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji
- VIII. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- IX. Kupokea, Kusikiliza na Kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi
- X. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- XI. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

4. MASHARTI YA JUMLA

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye Umri kati ya miaka 20 hadi 45
- II. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- III. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na Wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti walizonazo,

wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao

- IV. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (3) wa kuaminika.
- V. Maombi yote yaambatishwe na nakala za vyeti vya Taaluma na Vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na Vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia kazi husika. Pia unatakiwa kuambatisha picha ndogo (passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina nyuma yake
- VI. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results na Hati za Matokeo ya kidato cha Nne au Sita
HAVITAKUBALIWA
- VII. Waombaji waliosoma Nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- VIII. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana **kibali** cha Katibu Mkuu Kiongozi
- IX. Uwasilishaji wa sifa za **kughushi** Wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria
- X. Maombi yaandikwe kwa mkono na Mwombaji, kwa Lugha ya Kiswahili au kiingereza
- XI. Waombaji wote kwenye Barua zao za maombi waandike Namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano

XII. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ya Posta kama ifuatavyo:

Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 3
MATAI - KALAMBO

N:B Maombi yatakayowasilishwa kwa mkono hayatapokelewa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **04 Aprili, 2018 Saa 9:30 Alasiri**

Limetolewa na


Ephraim Moses

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
KALAMBO

**MKURUGENZI MTENDAJI WA W.L.P. 3
KALAMBO**